

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

Simu: +25526-230081
Nukushi: +25526-2321170
Barua pepe: km@habari.go.tz
Tovuti: www.habari.go.tz



S. L. P 25,
Mtaa wa Habari,
Mji wa Serikali Mtumba,
40481 Dodoma.

TAARIFA KWA UMMA

UTEUZI WA WATENDAJI WAANDAMIZI SEKTA YA SANAA

Dodoma – Machi 06, 2021

Umma na wadau wa sekta ya Sanaa unaarifiwa kuwa Wizara imekamilisha taratibu za uteuzi wa watendaji muhimu katika sekta ya Sanaa nchini.

Taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu wa Wizara, Dkt. Hassan Abbasi imeeleza kuwa walioteuliwa na nafasi zao ni kama ifuatavyo:

1. Dkt. Emmanuel Mwesiga Ishengoma ameteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Sanaa katika wizara hiyo.

Kabla ya uteuzi huo Dkt. Ishengoma alikuwa Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia Haki na Maendeleo ya Wasanii ambaye amekuwa pia akikaimu nafasi aliyothibitishwa sasa.

2. Dkt. Kiagho Bukheti Kilonzo ameteuliwa kuwa Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania (TFB).

Kabla ya uteuzi huo Dkt. Kilonzo alikuwa anakaimu nafasi hiyo katika Bodi ya Filamu akitokea Wizarani.

Uteuzi wa viongozi hao umeanza rasmi tarehe 01 Machi 2021 na wadau wa tasnia ya sanaa wanaombwa kuwapa ushirikiano stahiki wakati huu Serikali ikiendelea kufanya mageuzi makubwa katika sekta hiyo muhimu nchini.

Imetolewa na:

Eleuteri E. Mangi
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo